# BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

Simu Nam. + 255 24 2230602/1
Fax Nam. + 255 24 2230215
Tovuti: www.zanzibarassembly.go.tz

SANDUKU LA BARUA 902,
ZANZIBAR
Barua Pepe: zahore@zanlink.com

## HOTUBA YA MAONI YA KAMATI YA KUSIMAMIA OFISI ZA VIONGOZI WAKUU WA KITAIFA YA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR KUHUSU UTEKELEZAJI WA MAONI, USHAURI NA MAPENDEKEZO YALIYOTOLEWA NA KAMATI KATIKA MWAKA WA FEDHA 2021/2022 KWA OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA, SERIKALI ZA MITAA NA IDARA MAALUM ZA SMZ

---

**Mheshimiwa Spika,** kwa heshima kubwa naanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa kutujaalia uhai pamoja na afya njema ambavyo vimetuwezesha kukutana tena katika Baraza hili tukufu tayari kutekeleza majukumu yetu ya msingi kwa nchi yetu kwa ujumla. Ninamuomba Mwenyezi Mungu Mtukufu azidi kutukirimu neema zake ambazo kwa hakika sote ni wahitaji kwake.

**Mheshimiwa Spika,** napenda pia kukushukuru na kukupongeza wewe pamoja na wasaidizi wako, Mhe. Naibu Spika pamoja na Wenyeviti wa Baraza kwa namna mnavyoliendesha Baraza kwa umahiri mkubwa, namuomba Mwenyezi Mungu awazidishie hekma na busara katika jukumu lenu la kutuongoza ili tuweze kutekeleza vyema wajibu wa chombo hiki.

**Mheshimiwa Spika**, nitakuwa mchoyo wa fadhila iwapo sitowashukuru Wajumbe wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kwa namna

wanavyonipatia mashirikiano makubwa katika kutekeleza majukumu ya Kamati yetu.

**Mheshimiwa Spika,** nachukua fursa hii kuwatambua Wajumbe hao kama ifuatavyo:

| | | |
|---|---|---|
| *1.* | Mhe. Machano Othman Said | Mwenyekiti |
| *2.* | Mhe. Mtumwa Peya Yussuf | Makamu Mwenyekiti |
| *3.* | Mhe. Salma Mussa Bilal | Mjumbe |
| *4.* | Mhe. Mohamed Mgaza Jecha | Mjumbe |
| *5.* | Mhe. Zaina Abdulla Salum | Mjumbe |
| *6.* | Mhe. Suleiman Makame Ali | Mjumbe |
| *7.* | Nd. Ali Alawy Ali | Katibu |
| *8.* | Nd. Mwanaisha Mohammed Kheir | Katibu |
| *9.* | Nd. Amina Abeid Hemed | Mkalimani |

**Mheshimiwa Spika,** Kamati kwa kutumia Kanuni ya 107(3) inapewa jukumu la kufuatilia utekelezaji wa maoni na ushauri wa Kamati yaliyotolewa katika Ripoti ya Kamati ya mwaka uliotangulia. Ambapo kazi hii ilifanywa vyema kwa kipindi hiki kilichopita na bado Kamati inazidi kufuatilia utekelezaji wa maoni hayo kila inapoona inafaa kufanya hivyo.

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa kanuni ya *109(15)* ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi Zanzibar, imetoa fursa ya lazima kwa kila Kamati kutayarisha ripoti ya mwaka itakayowasilishwa katika kikao cha mwezi wa Februari cha Baraza la Wawakilishi Zanzibar kila mwaka.

**Mheshimiwa Spika,** aidha, Kanuni ya *109(17)* ya Kanuni za Baraza, inaelezea kuwa kabla ya kuwasilishwa Barazani utekelezaji wa maoni na ushauri huo, Kamati inatakiwa kukaa na wizara husika kujadili utekelezaji huo unaojumuisha maoni na ushauri wa Kamati kwa wizara na taasisi zake inazozifanyia kazi.

**Mheshimiwa Spika,** Hotuba hii inaelekeza kwa Wizara ya Nchi Ofisi ya Rais,

Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ ambapo jumla ya maoni na ushauri *36* yaliyopendekezwa na Kamati katika mwaka wa fedha *2021/2022* katika kuimarisha utekelezaji wa maagizo yake.

UTEKELEZAJI WA MAAGIZO:

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imefarijika sana na inatoa shukurani zake za dhati kwa Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ kwa jinsi walivyoweza kutekeleza vyema maagizo hayo hali inayoonesha ukomavu katika utekelezaji wake pamoja na jitihada njema za kuleta maendeleo nchini.

**Mheshimiwa Spika,** licha ya Wizara kutekeleza vyema maoni na ushauri uliotolewa na Kamati, kuna baadhi ya maoni na ushauri ambao Kamati imeitaka Wizara kufuatilia zaidi utekelezaji wa maoni hayo kwa kutoa maelekezo yafuatayo:

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inashauri kuanzishwa kwa vyanzo vipya vya mapato katika Halmashauri zote za Unguja na Pemba.

Wizara ifuatilie kwa ukaribu uibuaji na unazishwaji wa vyanzo vipya vya mapato katika Halmashauri zote ikiwemo Mabaraza ya Miji na Manispaa ili kuongeza kasi ya ukusanyaji wa mapato. Aidha, Wizara pia isimamie fedha za marejesho ambazo zimekuwa zikichelewa sana kutoka Idara ya Maliasili ziweze kupatikana kwa wakati ili kusaidia katika harakati za maendeleo ya Serikali za Mitaa.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inapendekeza Wizara Kuzisimamia Halmashauri, Mabaraza ya Miji na Manispaa kuhakikisha wameongeza nguvu katika kufanya usafi wa miji.

Kamati imeitaka Wizara kusimamia kwa karibu sana watendaji wa Halmashauri na Manispaa zetu kwa lengo la kudumisha usafi wa miji. Aidha, juhudi za

makusudi zinahitajika katika utafutaji wa magari ya kubebea taka na kuimarisha zoezi la uwekaji wa mapipa (dust bin) ya kuwekea taka sehemu zote za miji ili kurahisisha zoezi la usafi kwa wakaazi wa maeneo ya mji.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaishauri Wizara kuzisaidia Halmashauri zetu kupata vitendea kazi vya kisasa ili kwendana na wakati na mazingira halisi.

Kamati imeitaka Wizara kuzisaidia Halmashauri na mabaraza kuhakikisha wamekuwa na vitendea kazi vya kisasa ambavyo vitarahisisha majukumu yao. Vifaa hii vitajumuisha magari ya kufanyia kazi, mashine za ukusanyaji wa mapato na vifaa nyengine mbali mbali ambavyo ni muhimu kuwepo katika utendaji wao wa kila siku.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati katika ziara zake mbali mbali iligundua tatizo la uhaba wa wafanyakazi katika Halmashauri, jambo ambalo tayari mheshimiwa Raisi wetu mpendwa Dkt. Husein Mwinyi ameshalitolea ufafanuzi.

Kwa hivyo, Kamati inapendekeza Wizara kusimamia utaratibu wa upatikanaji wa wafanyakazi wa mkataba ambao watakua muhimu katika utekelezaji wa majukujmu ya Halmashauri zetu kwa upande wa Unguja na Pemba. Aidha, katika utekelezaji wa agizo hili Wizara uhakikishe wameajiri wataalamu ambao watazisaidia Taasisi hizi kufikia malengo yake.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imeelezwa na imebaini kuwepo kwa changamoto kubwa ya usajili na utoaji wa vitambulisho vya wajasiriamali.

Kamati imeishauri Wizara kupitia ofisi za Wakuu wa Mikoa kusimamia zoezi la usajili wa wajasiriamali pamoja na kuwaapatia vitambulisho ambavyo vitawapunguzia usumbufu katika shughuli zao. Katika kasi ya usajili na utaoaji wa vitambulisho hivi, Kamati haikuridhika na kuona baadhi ya Wilaya zimetoa idadi ndogo sana ukilinganisha na wajasiriamali waliopo katika maeneo mbali

mbali ya biashara. Kamati inashauri ikiwa wananchi wanalalamikia ukubwa wa gharama za vitambulisho basi iwepo njia mbadala ya kulipa kwa awamu au kupunguzwa kwa kiasi cha fedha ili kuruhusu idasi kubwa ya wajasiriamali kuweza kusajiliwa.

**Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa Utekelezaji wa Idara Maalum za SMZ:


*(a)* Kamati inazipongeza Idara Maalum kwa juhudi zao kubwa wanazochukua katika kuhakikisha nchi yetu ipo katika mikono salama na shughuli za kimaendeleo zinafanyika kwa Amani na utulivu.

*(b)* Aidha, Kamati inaishauri Wizara kutumia wataalamu wake wa mipango kufanya utafiti wa kina katika ukadiriaji wa fedha za makusanyo kwani iadara hizi huwekewa mafungu makubwa katika ukusanyaji wa mapato ambapo ni tofauti vyanzo wanavyotumia.

**Mheshimiwa Spika,** kwa kumalizia naomba kuchukua fursa hii tena kuishukuru Wizara kwa mashirikiano yake inayoipa Kamati katika kutekeleza majukumu yake na kuomba kuzidisha mashirikiano hayo ili kuweza kufikia lengo la Serikali kuleta maendeleo nchini.

**Mheshimiwa Spika,** naomba kuwasilisha.

Ahsante,



………………………………….

(Mhe. Machano Othman Said),

***Mwenyekiti,***

***Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa,***

BARAZA LA WAWAKILISHI,

ZANZIBAR